

Vitu Vinavyookoa

na

Coy Garrison

Vitu Vinavyookoa

na

Coy Garrison

Novemba 12, 2011

Vitu Vinavyookoa

Tunapongelea swala la kuokolewa, hatupaswi kuwa kama wale wanaoridhika kwa kusoma mustaro mmoja na kuacha maisha yetu yaliyobaki katika mustari husika. Nawafahamu watu wanaosoma Yohana 3:16 kana kwamba wanadhani kwamba ilikuwa ni andiko moja tu katika Biblia yote, na kwamba ilikuwa hitimisho ya Injili; hataivyo, Ninakubali kwamba maandiko yana hadithi kuu ambayo hajjawahi kutokea. Lakini kwa kusoma kifungu hiki kimoja, na kusema hakuna cha ziada kwangu, bali kuamini tu, itakuwa ni mauaji ya kiroho. Vitu tunavyotaka kuanzisha katika somo hili fupi ni kwamba kuna mengi zaidi ya kifungu hiki kimoja ambayo inahusiana na wewe na mimi ili tuokolewe. Haita kuwa na maana kumhukumu mfungwa kwa shahidi mmoja; ama sisi tuhukumu ao tujione hatuna hatia kwa kusoma kifungu kinachozungumzia upendo, kama ilivyoandikwa. Tafadhali, zingatia kwa muda, maandiko yafuatayo, ambayo pia ni maandishi ya Mungu; na uyapime wewe binafsi, kama ni ya kweli au hapana? Tunakumbushwa katika Yohana 8:32, “*Nanyi mtaifahamu kweli, na hiyo kweli itawaweka huru.*” Ningependa nisiwe na upendeleo, na nipende na wewe uchukue Biblia yako, na tusome kama ifuatavyo:

Mungu anatuokoa. 1 Tim. 4:10, “*Kwa maana twajitaabisha na kujitahidi kwa kusudi hili, kwa sababu tunamtumaini Mungu aliye hai, aliye Mwokozi wa watu wote, hasa wa waaminio.*” Hapa tutambua kuwa Muumbaji wetu pia ni Mwokozi wetu, maana ameifanya iwezekane kwetu kuokolewa.

Kristo anatuokoa. Mat. 1:21, “*Naye atazaa Mwana nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*”

Tunaokolewa kwa uhai wake. Rum. 5:10, “*Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tukaokolewa katika uzima wake.*”

Tunaokolewa kwa damu yake. Rum. 5:9, “*Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.*”

Tunaokolewa kwa Injili. 1 Kor. 15:1-2, “*Basi ndugu zangu nawaarifu ile injili niliyowahubiri; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri isipokuwa mliamini bure.*”

Tunaokolewa kwa neema. Efe. 2:8, “*Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu,*”

Tunaokolewa kwa imani. Rum. 5:1, “*Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.*”

Tunaokolewa kwa tumaini. Rum. 8:24, “*Kwa maana tuliokolewa kwa taraja; lakini kitu kilichotarajiwa, kikionekana hakuna taraja tena. Kwa maana ni nani anayekitarajia kile akionacho?*”

Tunaokolewa kwa matendo. Yak. 2:24, “*Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake; si kwa imani pekee yake.*”

Tunaokolewa kwa maneno. Hapa utaona kutoka katika maandiko kwamba Kornelio alisikia maneno kutoka, na kupitia maono. Mdo. 11:13-14, “*Akatueleza jinsi alivyomwona malaika aliyesimama nyumbani mwake na kumwambia, tuma watu kwenda Yafa ukamwite Simoni aitwae Petro, atakayekuambia maneno ambayo yatakuokoa, wewe na nyumba yako yote.*”

Tunaokolewa kwa kuliitia jina la Bwana. Rum. 10:13, “*Kwa kuwa kila atakayeliitia jina la Bwana, ataokoka.*”

Tunaokolewa kwa ubatizo. 1 Pet. 3:21, “*Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (sio kuweka mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo.*”

Kwa ye yote, na nimesoma somo hili fupi kutoka katika neno la Mungu, pia tunakumbushwa katika Mdo. 2:40, “*...jiokoeni nafsi zenu na kizazi hiki chenye ukaidi.*” Unaweza ukazingatia haya na maandiko mengine mengi ili kuweza kuamua ndani ya moyo wako? Tunapata kwamba watu fulani katika Mdo. 17:11, “*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*”

Kwa upendo wa Kristo,

Coy Garrison, *It Is Written*, Oktoba, 1951

